

SWALI NA. 4

ATCL — KUANZISHA SAFARI ZA NDEGE — ZANZIBAR — DODOMA MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BWZ) Atauliza:-

ATCL Corporation ni Shirika la Ndege la Serikali na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na limekuwa likifanya vizuri chini ya Uongozi wa Mkurugenzi Mkuu — Eng. Matindi:-

- (a) Je, kwa nini ATCL kila Jumatatu inapoondoka Dar es Salaam kwenda Dodoma isipitie Zanzibar ili Viongozi pamoja na Wananchi wanaotaka kwenda Dodoma wapate huduma hiyo;
- (b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa safari za ATCL kutoka Dar es Salaam zipitie Zanzibar kwa Jumatatu zote kupunguza tatizo la usafiri kwa Wananchi wa Zanzibar wanaotaka kwenda Dodoma kwa shughuli mbalimbali;
- (c) Je, ni lini safari hizo zitaanza ili Viongozi, Wananchi na Watalii kutoka Zanzibar waone kuwa Serikali yao inawajali na inadumisha Muungano wetu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Atajibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub Mbunge wa Konde lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:

- (a) Dhumuni la Serikali kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ni kuhakikisha wananchi wote wa Tanzania Bara na

Visiwani wanapata huduma ya usafiri wa anga kwenye kituo (destination) chochote chenye maslahi ya kibiashara. Aidha, ATCL inatumia kituo cha Dar es Salaam kama kitovu ili kuwa na muunganiko wa kupeleka abiria sehemu nyingi na kukidhi mizania ya kibiashara kwani bila kufanya hivyo inaweza kukosa abiria wa kutosha kutoka kituo kimoja kwenda kingine moja kwa moja. Kwa kuzingatia hilo, Serikali kupitia ATCL imebaini kuwa Zanzibar ni moja ya vituo ambavyo kuna maslahi kibiashara. Hivyo, imesharekebisha ratiba zake ili kuhakikisha wasafiri kutoka Zanzibar wanakuwa na uwezo wa kusafiri kwenda Dodoma kupitia kitovu (hub) cha Dar es Salaam kwa kuwa na ndege siku ya Ijumaa kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam ambapo abiria hao wataweza kuunganisha Safari kwenda Dodoma kwa ndege ya alasiri siku hiyohiyo ya Ijumaa. Aidha, ATCL ina ndege Jumapili inayotoka Zanzibar kuja Dar es salaam asubuhi ambayo itaunganisha na ndege inayokwenda Dodoma.

(b) Kama nilivyoeleza kwenye jibu la kipengele (a) cha swali hili, hivi sasa siyo wakati muafaka kwa kila Jumatatu ndege ya ATCL inapoondoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ipitie Zanzibar. Aidha, utaratibu huo wa safari za ATCL kutoka Dar es Salaam kupitia Zanzibar kwa kila Jumatatu utanza pindi muunganiko wa kupeleka abiria Zanzibar kutoka Dar es Salaam na sehemu zingine kwa siku ya Jumatatu utakidhi mizania ya kibiashara.

(c) Safari za ATCL kila Jumatatu kutokea Dar es Salaam kwenda Dodoma kupitia Zanzibar zitaanza pindi muunganiko wa kupeleka abiria sehemu zingine kupitia Zanzibar utakapokidhi mizania ya kibiashara. Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawajali Viongozi, Wananchi na Watalii kutoka Zanzibar na ndiyo maana inajitahidi kwa kila hali kuhakikisha kuwa Viongozi, Wananchi na Watalii kutoka Zanzibar wanapata usafiri wa kuunganisha kutoka kituo cha Dar es Salaam kama kitovu kwenda Dodoma kwa kadiri inavyowezekana.